

11

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 26 mwezi 03 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MPANDA, S.L.P. 190,  
MPANDA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

ALEX W. NYERERE S.L.P. 99, CHUNYA  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNYA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNYA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya KUFUNGA UMEME AWAMU YA PILI NA AWAMU YA TATU KATIKA MAJENGO YA CHUO CHA VETA CHUNYA.

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania TSHs. 15,000,000, Fundu atafanya kazi ya UMEME kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamia":5% ya Gharama ya Ufundi.

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 27 mwezi 03 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 18 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## 5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

**KUFINGA UMEME AWAMU YA PILI NA YA TATU**

- (a) \_\_\_\_\_ na kukamilisha kazi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHIURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA  
MPANDA

Jina: Joseph Mawanya Saini: [Signature]

Wadhifa: MKW WA CHUO Tarehe: 26/03/2022  
Principal  
Mpanda Vocational Training Centre  
P. O. BOX 190  
Mpanda

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ERASMUS ZUMBA Saini: [Signature]

Wadhifa: MWALIMU Tarehe: 26/03/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: ALEX W. NYERERE Saini: [Signature]  
Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: 26/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: MICHAEL JOSEPH Saini: [Signature]

Wadhifa: FUNDI MSAIDIZI Tarehe: 26/03/2022